# MUHTASARI

## Hali ya Kiutandawazi ya Mazao ya Kibiashara Yaliyogeuzwa Jeni Kibayoteki: 2010

**na Clive James, Mwanzilishi na Mwenyekiti wa ISAAA**

## *Mazao ya Kibayoteki Yasambaa zaidi ya Hekta Bilioni 1*

Mwaka 2010 ulikuwa ni ukumbusho wa Mazao ya kibayoteki yaliyofanywaya kibiashara, 1996-2010.

Mkusanyiko wa hekta kuanzia 1996 hadi 2010 zilizidi hekta bilioni 1(sawa na jumla ya eneo pana la Marekani au Uchina), hii inaonyesha dhahiri kuwa mazao ya kibayoteki itadumu.

Rekodi ya ongezeko la mara 87 kihekta kati ya 1996 na 2010, ambayo inaifanya teknolojia ya mazao ya kibayoteki iwe teknolojia inayokua haraka zaidi katika historia ya mazao badilifu ya kilimo cha kisasa.

Ukuaji wa nguvu, maradufu wa 10% katika 2010 uliofikia hekta milioni 148 - dhahiri, ni ongezeko la pili kubwa zaidi katika miaka 15. "Hekta Bainishi" zilikua kutoka hekta milioni 180 katika 2009, hadi hekta milioni 205 katika 2010, ongezeko la 14% au "hekta bainishi" milioni 25.

Idadi ya nchi zinazopanda mazao ya kibayoteki ziliongezeka mno hadi kufikia rekodi ya nchi 29, ongezeko la kutoka nchi 25 katika 2009 – kwa mara ya kwanza, nchi 10 zinazoongoza kila moja ilipanda hekta milioni 1. Zaidi ya nusu ya idadi ya watu ya ulimwengu, 59% au watu bilioni ~4, huishi katika nchi 29 zinazopanda mazao ya kibayotekii.

Nchi mpya tatu, Pakistan, Myanmari na Ususwi zilitoa taarifa rasmi ya kupanda mazao ya kibayoteki ikiwa mara ya kwanza katika 2010, naUjerumani ilirejelea kuyapanda tena.

Kati ya nchi za kibayoteki 29 katika 2010 nchi 19 zilikuwa nchi zinazoendelea na nchi 10 tu ndizo zilizokuwa za viwanda: kwa kuongezea, nchi zingine 30 ziliagiza bidhaa za mazao ya kibayoteki kwa kuwa jumla ya nchi 59 zimeidhinisha matumizi ya mazao ya kibayoteki, aidha kwa kupanda au kwa kuagiza kutoka nje; 75% ya idadi ya watu ulimwenguni huishi katika nchi hizo 59.
Katika 2010, rekodi ya wakulima milioni 15.4 walipanda mazao ya kibayoteki dhahiri zaidi ya asilimia 90% au milioni 14.4 walikuwa wakulima maskini wasio na mtaji waliko kwenye nchi zinazoendelea; idadi ya wakulima haijabadilika kutokana na faida zinazotokana na mazao ya kibayoteki kwa mazao mapya ya kijadi. Inashangaza, kuanzia 1996, wakulima pote ulimwenguni walichagua kutoa maamuzi huru - milioni ~100 ya kupanda na kupanda tena zaidi mazao ya kibayoteki kila mwaka, kwa sababu ya faida zake muhimu.

Nchi zinazoendelea zililima 48% ya mazao ya kibayoteki kiutandawazi katika 2010 na zitazidi ukubwa wa kihekta nchi za viwanda kabla ya 2015 kiwango cha ukuaji wa kibayoteki ulikuwa wa haraka zaidi katika nchi zinazoendelea. Asilimia 17% au hekta milioni 10.2, dhidi ya 5% au hekta milioni 3.8 ya nchi za viwanda.

Nchi tano zinazoendelea zinazoongoza katika mazao ya kibayoteki ni, Uchina na India katika Asia, Brazili na Ajentina katika Amerika Kusini, na Afrika Kusini katika bara la Afrika.
Brazili, mfano wa ukuaji katika Amerika Kusini, iliongeza hekta zake za mazao ya kibayoteki zaidi ya nchi yoyote ulimwenguni kote - ongezeko la hekta milioni 4.

Katika Australia mazao ya kibayoteki yamefufuka baada ya ukame wa mpigo na kuwa na ongezeko kubwa zaidi la mazao ya kibayoteki kuliko nchi nyingine yoyote ulimwenguni – rekodi ya ongezeko la hekta milioni 4.

Katika Australia, mazao ya kibayoteki yamefufuka baada ya ukame mkubwa wa mwaka mzima kwa kuwa kiwango kikubwa zaidi cha ongezeko la mwaka hadi mwaka la 184% na kufikia hekta 653 elfu.

Bukina Faso ilikuwa na kiwango kikubwa cha pili cha ongezeko la hekta za kibayoteki kwa 126% na kuwa na wakulima 80 elfu waliolima rekodi ya hekta 200 elfu ambazo ni sawasawa na kiwango cha kibali 65%.

Katika Myanmari, wakulima wadogo 375% walifanikiwa kupanda hekta 275 elfu za pamba kibayoteki, sawasawa na 75% ya ukubalifu wa kibayoteki pamba yote inayolimwa katika nchi hiyo.

Katika India, ukuaji wa stellar uliendelea kwa miaka tisa, na wakulima milioni 6.3 wakilima hekta milioni 9.4 za pamba kibayoteki , sawasawa na kiwango cha ukubalifu wa 86%.

Meksiko ilifanikiwa kufanya majaribio ya kwanza shambani ya mahindi ya kibayoteki.

Rekodi ya nane ya Muungano wa Nchi za Ulaya(EU), zililima aidha mahindi ya kibayoteki au "Amflora", kiasi cha kiwango, kilichoidhinisha upya na Muungano wa Nchi za Ulaya – uidhinishaji wa kwanza katika miaka 13 ya kulima katika Muungano wa Nchi za Ulaya.

Kwa mara ya kwanza, mazao ya kibayoteki yalichukuwa ukubwa wa 10% ya – hekta bilioni ~1.5 ya eneo la upanzi kiutandawazi; >50% ya eneo la upanzi la kiutandawazi iko kwenye nchi ishirini na tisa zinazopanda mazao ya kibayoteki 2010.

Sifa bainishi ni muhimu kwa mazao ya kibayoteki kwa siku zijazo – nchi 11 zilipanda mazao ya kibayoteki yenye sifa bainishi mbili au zaidi katika 2010; na nane zilikuwa ni Nchi zinazoendelea – hekta milioni 32.2 au 22% ya hekta milioni 148 za pamoja katika 2010.

Kuanzia 1996 hadi 2009, mazao ya kibayoteki yalichangia Uimarishaji na Uendelevu wa Mabadiliko ya Hali ya Hewa kwa: kuongezea uzalishaji wa mazao na thamani kwa dola za Marekani bilioni 65; na kuleta mazingira bora zaidi, kwa kuokoa kilo milioni 363 za dawa za kunyunyuzia wadudu; katika 2009 pekee yake na kupunguza utoaji wa hewa ya karboni kwa kuokoa kilo bilioni 18 zilizo sawa na kuondoa magari milioni ~8 barabarani; na kuhifadhi Viumbe hai kuokoa hekta milioni 75 za nchi; na kusaidia kupunguza umaskini kwa kuwasaidia wakulima wadogo ambao ni kati ya watu maskini zaidi duniani.

Kuna mahitaji ya dharura ya kuwa na kanuni za marekebisho zinazofaa za gharama/muda- ambazo zinawajibika, kwa nguvu lakini si za kutaabisha, kwa ajili ya nchi ndogo na maskini zinazoendelea.

Thamani ya pekee ya mbegu za kibayoteki kiutandawazi zilikuwa na thamani ya dola za Marekani bilioni 11.2 katika 2010, pamoja na mahindi ya kibayoteki, maharage ya soya, na pamba za thamani ya dola za Marekani bilioni ~150 kwa mwaka.

Matumaini ya Baadae yanatia moyo kwa miaka mitano ijayo: mahindi yanayohimili ukame katika 2012; mchele wa kikahawia katika 2013; mchele wa kibayoteki kabla ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya 2015, kuweza kunufaisha watu maskini bilioni 1 kwenye kaya za walima mchele, katika Asia peke yake mazao ya kibayoteki yanaweza kutoa mchango mkubwa kwenye Malengo ya Maendeleo ya Milenia ya 2015 ya kupunguza umaskini kwa nusu, kwa kuboresha uzalishaji wa mazao kwenye uanzilishi wa kiutandawazi uliokusudiwa ili kumkirimu Mshauri na Mwanzilishi wa ISAAA Mshairi na Mshindi waTuzo la Amani la Nobeli, Norman Borlaug, ambaye aliokoa watu bilioni 1 kutokana na njaa.

Habari kwa urefu zitatolewa kwenye muhtasari wa 42 wa "Hali ya Kiutandawazi ya Mazao ya Kibiashara Yaliyogeuzwa Jeni Kibayoteki; 2010,'' zilizochapishwa na Clive James. Kwa habari zaidi, tafadhali angalia http://www.isaaa.org au wasiliana na ISAAA SEAsia Center kwenye +63 49 536 7216, au barua pepe info@isaaa.org. Au na ISAAA AfriCenter katika +254 20 4223618, au baruapepe kwa africenter@isaaa.org.